

Wafugaji wa kuku wa nyama, mayai wasiosajiliwa kuchukuliwa hatua

□ NA ASHURA ASSAD

WAFUGAJI wa kuku wa nyama na mayai wametakiwa kujisajili kisheria ili waweze kutambulika na kufanya kazi ya ufugaji kwa kufuata sheria zilizowekwa.

Imeelezwa kuwa wale wote ambao hawajasajiliwa, lakini wanafanya kazi ya ufugaji kuku, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mtafiti Mkuu na Mratibu wa Ufugaji Kuku kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. John Kaijage, alisema wafugaji wote wanatakiwa kusajiliwa kisheria ili kupunguza wimbi la wafugaji wanaofuga kuku kwa kutumia mazoea.

Alisema mpaka sasa wafugaji wa kuku waliosajiliwa na kutambulika ni 41, huku wafugaji wa kutotoresha vifaranga

wakiwa 78 na wengine wanafanya kazi hiyo bila kutambulika.

Kaijage alisema lengo la usajili huo ni kuwakusanya wafugaji wa kuku na kuwapatia elimu itakayokuwa endelevu sanjari na kuwasajili ili watambulike kisheria na kupata soko zuri la ndani na nje ya nchi.

"Tunataka kila mfugaji wa kuku wa nyama na mayai awe na kitambulisho chake cha usajili ili aweze kufanya kazi kwa uhakika. Kwa wale ambao wanauza kuku na mayai, wanatakiwa kuwa na vitambulisho vyao ili wanunuzi wao wajue kama wamesajiliwa," alisema.

Pia, alitoa rai kwa taasisi za kifedha kupunguza riba kwa wajasiriamali wadogo ili wawasaidie kukuza mitaji yao kwa sababu riba kubwa ina changamoto kwenye shuhuli zao.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama cha Ufugaji Kuku wa Nyama na

Mayai, Aloyce Makoye, alisema wafugaji wa kuku wanakumbwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo ya ukosefu wa mitaji na ukosefu wa elimu ya ufugaji wa kuku na nyama.

Makoye alisema elimu ya ufugaji wa kuku wa nyama na mayai bado iko nchini, hali inayosababisha watu kujifugia waliyozoea na kusababisha hasara za mara kwa mara.

"Utakuta mtu anafuga kuku wa nyama na mayai, lakini hana elimu ya aina yoyote, hata ikitokea wale kuku wameumwa, anaishia kuwashinja, badala ya kuwatafutia dawa za kitaalamu na kuwatibu," alisema.

Alifafanua kuwa mikopo mingi ina changamoto kwa sababu ya riba kubwa, hali inayowafanya washindwe kurudisha marejesho ya mikopo huku taasisi za mikopo zikikataa kuwakopesha.

10

Ndaki ataka viwanda vya kuchakata samaki kuangalia bei zenye tija

Na Edward Kondela, Mwanza

■ ■ ■ SERIKALI imesema itahakikisha sekta za mifugo na uvuvi zinawaondoa wananchi katika umasikini, kupata ajira na nchi iweze kuza bidhaa bora za mazao ya mifugo na uvuvi ndani na nje ya nchi.

Akizungumza jana katika siku yake ya kwanza ya ziara ya kikazi ya siku mbili mkoani Mwanza Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki wakati akihitimisha ziara hiyo kwenye kiwanda cha kuchinja na kuchakata nyama cha Chobo kilichopo Kata ya Usagara Wilaya ya Misungwi amesema wizara imekuwa ikichukulia kwa uzito mkubwa suala la viwanda ambalo litaweza kubadilisha fikra za wafugaji na wavuvi.

"Wananchi wetu waondoo umaskini, wananchi wetu wapate ajira na siku tuze bidhaa za mazao haya ya mifugo na uvuvi yaliyo bora hapa ndani na kule kwa wenzetu nje, sasa mimi nikikuta hali ya mikwamo kwa kitu ambacho kinatusaidia kuelekea huko napata shida," alisema Waziri Ndaki.

Waziri Ndaki akifuatana na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul katika ziara hiyo alifatanua kuwa haridhishwi na baadhi ya changamoto wanazokutana nazo wawekezaji ambao wamejikita katika kuyaongezesha thamani mazao

ya mifugo na uvuvi.

Alimuagiza Kaimu Msajili wa Bodi ya Nyama, Iman Sichalwe kumpatia taarifa ya hali ya viwanda vya nyama nchini ili apate tathmini halisi ya utendaji kazi wa viwanda hivyo na kuhakikisha inafuatilia changamoto zinazohusu wizara hiyo ili kuzipatia majibu.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda hicho, John Chobo alisema kwa sasa kiwanda chake kimesimamisha uzalishaji na kinatarajia kuanza kurejea katika shughuli zake Januari, 2021 baada ya ugonjwa wa Covid 19 kuathin shughuli za kiwanda hicho ambacho kimekuwa kikisambaza nyama katika nchi za falme za kiarabu.

Chobo amesema kutopatikana kwa taarifa sahihi za mifugo kumekuwa kukichangia kwa kiasi kikubwa soko la nyama kutoka Tanzania kwenda nje ya nchi kuwekwa katika daraja la chini kwa kuwa mifugo mingi ambayo inachakatwa viwandani haina taarifa sahihi juu ya ukuaji wake, magonjwa na chango mibalimbali ambazo mifugo huo umepatiwa.

Akiwa katika kiwanda cha kuchakata samaki Nile Perch kilichopo eneo la viwanda katika Kata ya Nyakato Wilaya ya Nyamagana jijini Mwanza Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki akiambatana na Naibu

Waziri Pauline Gekul amewataka wawekezaji wa viwanda vya samaki vinyopo mkoani Mwanza kuhakikisha wanatumia usafiri wa ndege kutoka katika kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Mwanza kusafirisha minofu ya samaki ili kutangaza bidhaa zinazotengezwa hapa nchini.

Tungependa kuona usafirishaji wa minofu ya samaki unafanyika hapa nchini kwetu, badala ya nchi jirani kwa kusafirisha kwa maloni kwenda nchi za jirani, kuna uwezekano kabisa wa kutoa minofu ya samaki kutoka kiwanja cha ndege cha Mwanza kwenda nje ya nchi badala ya kutumia nchi za jirani," alisema.

Aliwataka wawekezaji wa viwanda vya samaki kuangalia namna ya kuongeza bei ya kununulia samaki kwa wavuvi wanaopeleka samaki katika viwanda hivyo ili wavuvi hao waweze kubadilisha maisha yao na kunufaika kupitia Sekta ya Uvuvi.

Waziri Ndaki aliyasema hayo baada ya Meneja Mkuu wa Kiwanda cha kuchakata samaki cha Nile Perch, Rupesh Mohan kumueleza Waziri Ndaki na Naibu Waziri Gekul kuwa viwanda vya samaki vimekuwa vikosa malighafi ya kutosha kutokana na soko la ndani kukua na wakati mwingine kupata samaki kwa bei ya juu, hali iliyomlazimu Waziri Ndaki

kubainisha kuwa kama bei ya soko la ndani imepanda ni dhahiri wavuvi watauzua samaki katika soko hilo badala ya kupeleka viwandani ambapo wanauza kwa bei ndogo.

Hivyo amevitaka viwanda vya kuchakata samaki kuangalia upya bei ya samaki wanayonunua ili wavuvi nao waweze kunufaika na kuboresha maisha yao na viwanda pia viweze kupata malighafi za kutosha.

Pia Waziri Ndaki alitembelea kiwanda cha kukausha mabondo ya samaki cha Hong Lin International Ltd kilichopo Wilaya ya Ilemela jijini Mwanza na kufurahishwa na kiwanda hicho kwa kutumia kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Mwanza kusafirisha bidhaa zake kwenda nchi za nje.

Naye Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Wang Shenghong ameishukuru serikali kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji hali inayomwezesha kufanya shughuli zake bila matatizo huku akiomba pia baadhi ya tozo zipunguzwe.

Katika siku ya kwanza ya ziara yake Mkoani Mwanza, Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Mashimba Ndaki akiwa na Naibu Waziri, Pauline Gekul wametembelea pia Maabara ya Taifa ya Uvuvi, Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi nchini (FETA) na Kituo cha Ulirzi wa Rasilimali za Uvuvi (FRP).

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki akiwa na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Pauline Gekul, wakati walipofanya ziara ya kikazi katika Maabara ya Taifa ya Uvuvi iliyopo Kata ya Nyegezi Wilaya ya Nyamagana Mkoani Mwanza na kushuhudia namna maabara hiyo inavyofanya kazi kwa kufanyia uchunguzi sampuli za samaki kutoka viwandani. Wa kwanza kushoto ni Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Uvuvi, Dkt. Rashid Tamatamah. (Picha na Edward Kondela)



luru

isho
uma,
isho
simu
nyika
cha
ncos
ayani

ia ya
okoni
a sh.
katika
u wa

di ya
okiwa
kuwa
netoa
no ya
rafasi
a nchi
io wa
nafasi

litumia
runuzi
ingatia
va na
ughuli
ikezo
andika
tinada
rosho,
runuzi
zadi ya

naombi
ihinda
ya juu
ya chini
lo moja
ama na

Ofisa
nduru,
katika
2,629,
mnada
na bei
ojumla
ataraja
nguko
baada
nti za
amilika
la.
ba ya
u cha
Vawa,
nduru
asibu
asiano

ujenzi wa Darala la Kigongo-Busisi lenye urefu wa Kilomita 3.2, mkoani Mwanza juzi.

HASARA LEO UK-14 - 30/12/22



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (wa pili kushoto), Naibu Waziri wake, Pauline Gekul (wa pili kulia) pamoja na Katibu Mkuu wa wizara hiyo (Uvuvi), Dk Rashid Tamatamah (kushoto) wakiangalia samaki walipotembelea kiwanda cha Nile Perch Nyamagana, Mwanza jana. (Picha na Wizara ya Mifugo na Uvuvi).

PICHA YA SIKU: UCHAKATAJI SAMAKI

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (wa pili kushoto), akiwa na naibu waziri wake, Pauline Gekul (wa pili kulia) pamoja na katibu mkuu wa wizara hiyo, Dk Rashid Tamatamah (kushoto), wakiangalia hatua za uchakataji wa samaki katika Kiwanda cha Nile Perch kilichopo Kata ya Nyakato, Wilaya ya Nyamagana jijini Mwanza juzi, walipotembelea kiwanda hicho. Picha na Mpigapicha Wetu



yo
o-
aji
s-
si
li-
ni

ir
za
ia
ca
ca
ro

la
ra
ro
ra
zi
u
a
la
r-
a
u
o

MWANANCHI HK-2 30/12/2020

Garden

BUSINESS

REGISTRATION

SA's competition watchdog approves Google, Fitbit deal

JOHANNESBURG

South Africa's regulator, the Competition Commission (Competition), has conditionally approved the proposed merger whereby Google intends to acquire Fitbit. In a statement, the competition watchdog says this is a global merger, notified in several jurisdictions, including the EU, US, Australia, Canada and Japan.

It notes that Google is active in a wide range of areas, including online search, online advertising, other online services such as YouTube, Google Maps and Gmail as well as cloud computing services. In addition, says the Commission, Google maintains and develops the Android ecosystem which includes an open source mobile operating system (OS) and a suite of mobile apps and services.

"Google's business in South Africa relates to the provision of local support and marketing services, internally for Google. Google does not sell any wearable devices or hardware in South Africa. The main products and services relevant to this transaction are Wear OS, Google Fit, The Play Store, Google Search and Google Ads," the regulator says.

It points out that Fitbit develops,


It explains that Android is a dominant mobile OS and unlike the Apple ecosystem it is not vertically integrated into the production of wear-worn wearable devices prior to the merger.

This makes Android an important input for third-party smartwatch manufacturers that compete with Fitbit, bearing in mind the integral connectivity between smartwatches, computer apps, to the wrist worn wearable device as well as smartphones, and given the significant market shares enjoyed by Android, the proposed merger will give Google the ability to exclude competitors of Fitbit or frustrate the functionalities of competitors' computer apps from operating optimally on Android OS.

"This will significantly alter the market structure for the supply of wrist-worn wearable devices in SA and increase barriers to entry for potential entrants in the market," the watchdog says. The Commission was also concerned that as a direct result of the proposed merger, Google will entrench its dominance in the online advertising and online search market.

"As a direct result of the proposed merger, Google would acquire (i) the database maintained by Fitbit about its users' health and fitness

Livestock dealers earn windfall as sales surge by 100bn/- in Q3



Cattle being sold at Paga livestock auction market in Dar es Salaam.

By Francis Kajulu

LIVESTOCK dealers had a field day during the third quarter of the year when sales surged by over 100bn/-. Bank of Tanzania has said.

In its Consolidated Zonal Economic report for the year ended September 2020, the Central Bank said value of livestock comprising of cattle, goats and sheep sold in registered markets increased by 31.4 percent to 475.85bn/- up from 362.23bn/- made in a similar period last year.

"This outturn was largely associated with the increase in demand in the domestic market and neighbouring countries. Cattle which contributed 90 percent of the total sales, registered a 30 percent increase, driven by price increase," the BOT report said.

The report further noted that Central and Dar es Salaam zones continued to account for the largest shares of livestock sales during the period under review. The Central Zone which comprises of Dodoma, Singida and Tabora regions led the pack with sales amounting to 126.04bn/-

up from 110.34bn/-. Dar es Salaam came second on the list with sales amounting to 110.58bn/- up from 81.5bn/- last year.

The report shows that the percentage share of value of livestock sold on registered market continued to stabilize with the Central Zone leading at 27 percent while Dar es Salaam had 23 percent.


The Northern Zone nearly doubled its value of sales to 102.57bn/- from 62.44bn/- during the period while Lake Zone had incredible sales amounting to 96.97bn/- up from the 75.57bn/-.

The South Eastern and Southern Highlands Zone performed fairly with a slight increase of sales compared to last year's figures. South Eastern Zone contributed only 0.1 percent of this year's value of sales while the Southern Highlands accounted for 4.6 percent of the sales.

According to the Ministry of Livestock and Fisheries data, in total, cattle increased from 32.2 million to 33.4 million, goats also increased from 20 million to 21.20 million while sheep increased to 5.65 million from 5.5 million.

BULLISH

Livestock dealers earn windfall as sales surge by 100bn/- in Q3



Cattle being sold at Pugu livestock auction market in Dar es Salaam.

By Francis Kajubi

LIVESTOCK dealers had a field day during the third quarter of the year when sales surged by over 100bn/-. Bank of Tanzania has said.

In its Consolidated Zonal Economic report for the year ended September 2020, the Central Bank said value of livestock comprising of cattle, goats and sheep sold in registered markets increased by 31.4 percent to 475.85bn/- up from 362.23bn/- made in a similar period last year.

"This outturn was largely associated with the increase in demand in the domestic market and neighbouring countries. Cattle which contributed 90 percent of the total sales, registered a 30 percent increase, driven by price increase," the BoT report said.

The report further noted that Central and Dar es Salaam zones continued to account for the largest shares of livestock sales during the period under review. The Central Zone which comprises of Dodoma, Singida and Tabora regions led the pack with sales amounting to 126.04bn/-

up from 110.34bn/-. Dar es Salaam came second on the list with sales amounting to 110.58bn/- up from 81.51bn/- last year.

The report shows that the percentage share of value of livestock sold on registered market continued to stabilize with the Central Zone leading at 27 percent while Dar es Salaam had 23 percent.

The Northern Zone nearly doubled its value of sales to 102.97bn/- from 62.44bn/- during the period while Lake Zone had incredible sales amounting to 96.91bn/- up from the 75.57bn/-.

The South Eastern and Southern Highlands Zone performed fairly with a slight increase of sales compared to last year's figures. South Eastern Zone contributed only 3.6 percent of this year's value of sales while the Southern Highlands accounted for 4.6 percent of the sales.

According to the Ministry of Livestock and Fisheries data, in total, cattle increased from 32.28 million to 33.4million; goats also increased from 20 million to 21.29 million while sheep increased to 5.65 million from 5.5 million.

Watakiwa kuitumia Taliri kufanya ufugaji wa kisasa

WAFUGAJI katika wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma wametakiwa kutumia Kituo cha Utafiti wa Mifugo (TALIRI), kujifunza juu ya ufugaji bora na wenye tija.

Imeelezwa kuwa ni vyema wafugaji wakajifunza kuwa na mifugo michache yenye tija kuliko kuwa na mifugo mingi isiyokuwa na tija wala kuwabatilisha kiuchumi.

Kauli hiyo imetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri wakati akizungumza na wafugaji wa Kata ya Luhundwa.


Alisema kwamba katika ziara yake hiyo amegundua kuwa bado wananchi wengi

wanafuga kizamani kwa kuwa na mifugo mingi isiyokuwa na tija na hiyo inatokana na kutotumia kituo cha utafiti wa mifugo cha Taliri kujipatia elimu ya ufugaji bora na wa kisasa.

"Inasikitisha kuona kituo cha TALIRI kinawafaidisha wafugaji kutoka nje ya Mpwapwa huku hapa wilayani bado wanafuga kienyeji, inasikitisha sana," alisema Shekimweri

Alisema serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na

Rais John Magufuli imejikita kuhakikisha wafugaji wanabatilika na kufuga kisasa ili



waweze kunufaika kiuchumi kwa kuwa na mifugo michache yenye tija na manufaa.

"Unakuta zizi lina ng'ombe 400 ambao wamekonda na ha-

wana ubora wakati angeweza kuwa na ng'ombe 100 wenye uzito mkubwa ukiangalia mifugo iliyopo Taliri inavutia kwa ukubwa na uzito. Sasa mifugo kama ya Taliri nataka kuiona kwa wananchi huko vijijini iwabadilishe kimaisha na kiuchumi," alisema Shekimweri

"Sasa niwaagize maofisa mifugo Kata zote kuwapitia wafugaji na kuwaangalia ufugaji wao na kuwapatia elimu ya ufugaji bora na wenye tija na pia muanzishe daftari la mifugo katika Kata zote ili kuweza kujua kila Kata ina mifugo kiasi gani na changamoto zinazo wakabili wafugaji," alisema mkuu huyo wa wilaya.

HABARI LEO uk.5 - 30/12/2020

Mashimba apania kuipaisha sekta ya mifugo, uvuvi

Na MWANDISHI WETU, Mwanza

SERIKALI imesema itahakikisha sekta za mifugo na uvuvi zinawaondoa wananchi katika umasikini, kutengeneza ajira na nchi kuuza bidhaa bora zitokanazo na sekta hizo na nje ya nchi.

Akizungumza jijini Mwanza, jana, wakati akiwa kwenye ziara ya kikazi mkoani humo, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, aliyetembelea Kiwanda cha Kuchinja na Kuchakata Nyama cha Chobo, kilichopo Usagara, Wilaya ya Misungwi, alisema wizara imekuwa ikichukulia kwa uzito mkubwa suala la viwanda, ambalo litaweza kubadilisha fikra za wafugaji na wavuvi.

"Wananchi waondoe umasikini, wapate ajira na sisi tuuze bidhaa za mazao haya ya mifugo na uvuvi yaliyo bora ndani na kule kwa wenzetu nje, sasa mimi nikikuta hali ya mkwamo kwa kitu ambacho kinatusaidia kuelekea huko, napata shida," alisema Waziri Ndaki.

Waziri Ndaki, aliyeongozana na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline

Gekul, alisema haridhishwi na baadhi ya changamoto wanazokutana nazo wawekezaji, ambao wamejikita katika kuyaongezea thamani mazao ya mifugo na uvuvi.

Alimuagiza Kaimu Msajili wa Bodi ya Nyama nchini, Iman Sichaile, kumpatia taarifa ya hali ya viwanda vya nyama nchini, ili apate tathmini halisi ya utendaji kazi wa viwanda hivyo, baada ya Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda cha Chobo, John Chobo, kubainisha baadhi ya changamoto, ambazo Waziri Ndaki alisema wizara itahakikisha inazifuatilia ili kuzipatia majibu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda hicho, Chobo, alisema kwa sasa kimesimamisha uzalishaji na kinatarajia kuanza kurejea katika shughuli zake, Januari, 2021, baada ya ugonjwa wa covid-19 kuathiri shughuli za kiwanda hicho.

Akiwa katika Kiwanda cha Kuchakata Samaki cha Nile Perch, kilichopo eneo la viwanda, Kata ya Nyakato, Wilaya ya Nyamagana, jijini Mwanza, Waziri Ndaki, aliwataka wawekezaji wa viwanda vya samaki vilivyopo mkoani humo, kuhakikisha

wanatumia usafiri wa ndege kutoka katika kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Mwanza, kusafirisha minofu ya samaki ili kutangaza bidhaa zinazotengezwa Tanzania.

"Tungependa kuona usafirishaji wa minofu ya samaki unafanyika hapa nchini kwetu, badala ya nchi jirani, kwa kusafirisha kwa malori kwenda nchi za jirani, kuna uwezekano kabisa wa kutoa minofu ya samaki kutoka kiwanja cha ndege cha Mwanza kwenda nje ya nchi, badala ya kutumia nchi za jirani," alifafanua.

Pia, Waziri Ndaki alitembelea kiwanda cha kukausha mabondo ya samaki cha Hong Lin International Ltd, kilichopo Wilaya ya Ilemela, jijini Mwanza na kufurahishwa na kiwanda hicho kutumia kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Mwanza, kusafirisha bidhaa zake kwenda nchi za nje.

Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Wang Shenghong, alishukuru serikali kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji, hali inayomuwezesha kufanya shughuli zake bila matatizo, huku akiomba pia baadhi ya tozo zipunguzwe.



KUHUS

Wakala wa chini ya W Serikali Sur usalama wa Wakala huz zilizohifadhi Wakala unat hayo yatauzi

NA	
1	Arush
2	Dodo
3	Kipaw
4	Maka
5	Songv
6	Shiny
7	Songe
8	Sumb

- Mahin Wareh
- Mnuni za kaz mahin kiasi c
- Mnuni mahin
- Mnuni maom
- Wakal. kuzing husika

Hiwo Waka

ZIARA YA KIKAZI



WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki na Naibu Waziri wake, Pauline Gekul, wakilangalia mabondo ya samaki yaliokaushwa kwa ajili ya kusafirishwa nje ya nchi, katika kiwanda cha kukausha mabondo ya samaki cha Hong Lin International Ltd, wilayani Ilemela, jijini Mwanza, jana. (Picha na Wizara ya Mifugo na Uvuvi).